HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

# KILIMO BORA CHA CHAINIZI KABICHI



## CHAINIZI KABICHI

**(*Brassica oleracea* var. *chinensis*)**

### UTANGULIZI:

Chainizi kabichi ni zao la mboga ambalo hustawi msimu wa baridi kati ya nyuzijoto 15-21. kiasi hiki cha joto ndicho kinachowezesha majani kwa zao hili. Zao hili likikomaa majani yake ya nje huchumwa kwa mfululizo muda mrefu.

Ni mboga inayopedwa na wengi na pia hupandwa kwa wingi katika bustani za wakulima wa Manispaa ya Ubungo.

### KUPANDA:

- Mbegu hustawishwa kwenye kitalu/ viriba maalumu.
- Baada ya wiki 4 huhamishiwa na kupandikizwa kwenye bustanini.

### UTAYARISHAJI WA ENEO LA KUPANDA:

- Tayarisha shamba kwa kufuata hatua zifuatazo:
- Katua shamba na vunja vunja mabonge ili kulainisha udongo.
- Ongeza mbolea ya kuku iliyooza au samadi/mbolea vunde na sawazisha kwa kutumia reki.
- Hamisha miche kutoka kwenye kitalu na pandikiza kwa kutumia nafasi ya sentimita 30—40 mche hadi mche. Na sentimita 30—45 mstari na mstari.

### MATUNZO:

### MAJI:

- Mwagilia maji kila siku, asubuhi na jioni

Udongo:

- Chainizi kabeji hustawi vizuri kwenye udongo rutuba, mboji mbolea nyingi na usiotuamisha maji.

### MBOLEA:

- Ongeza mbolea ya kuku iliyooza kila shimo, kiasi cha viganja viwili.

### WADUDU NA MAGONJWA:

- Magonjwa:
- Madoa jani (leaf spot)
- Kuoza kwa shina
- Magonjwa haya huzuiwa kwa kunyunyiza dawa za viwandani. Unashauriwa kuonana na mtaalam aliye karibu nawe

### WADUDU:

Nondo, funza wa inzi, viwavi, wadudu mafuta. Wadudu mafuta hunyonya maji ya mmea na viwavi hula majani.

- Wadudu hao hupunguza mazao na huathiri ubora wa majani.

### KUZUIA NA KUDHIBITI:

- Kagua shamba mara kwa mara ili kugundua mashambulizi mapema.
- Tumia mwarobaini
- Vile vile dawa za viwandani zitumike kudhibiti wadudu.
- Tumia dawa aina ya Decis, corragen & belt

### KUVUNA:

Baada ya siku 30 na kuendelea

### FAIDA YA MBOGA HII KATIKA LISHE YA BINADAMU

Ina viini lishe vya kiwango cha juu, na hasa huambatanishwa na chakula cha wanga.

Mboga hii ni chanzo kizuri cha vitamini A na C, na kwa kiasi kidogo ina vitamin K. Kuna madini chokaa (calcium), Phosphorus na Potassium. Mboga hii pia ina nyuzinyuzi ambazo husaidia usagaji wa chakula na hasa katika utumbo mkubwa, kuweka uwiano mzuri wa kiasi cha sukari na rehemu katika damu.

Mboga hii inatakiwa kuoshwa vizuri inapotoka shambani na kupikwa kabla haijanyauka ili kutopoteza virutubishi.

## Mapishi ya Chainizi kabichi

- Osha kwa maji ya kutosha kutoa uchafu wote
- Katakata vipande visiwe vidogo sana
- Weka sufuria jikoni, tia maji kidogo (1/4 Kkikombe), chumvi na mafuta kidogo sana
- Maji yakichemka, weka mboga uli-yoitayarisha, funika na geuza baada ya dk 3 ongeza nyaya na kitunguu (kama utapenda), acha ichemke kwa dakika 7 tena,
- Mboga hii huweza kupikwa pia kwa nazi au karanga
- Geuza na ipua tayari kwa kuliwa

**Kumbuka**

Mboga huliwa mara baada ya kupikwa na hairudiwi kupashwa kwani yaweza kupoteza virutubishi kwa wingi.

Kwa maelezo zaidi onana na wataalamu ofisi ya Kilimo Manispaa au ofisi za Kata.

Kimetayarishwa na:

IDARA Y A KILIMO, UM-WAGILIAJI NA USHIRIKA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA

UBUNGO

S.L.P. 55068,

DAR ES SALAAM.

Simu: 0222-926341

Fax: 0222-926342

Tovuti: www.ubungomc.go.tz

Barua pepe:info@ubungomc.go.tz

"kilimo,mifugo na uvuvi kwa ukuaji wa uchumi wa nchi"

"

"